JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2022

## KISWAHILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2022

## 01 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P.2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

**YALIYOMO**

DIBAJI ..................................................................................................... iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

1.1 SEHEMU A: Kusikiliza Hadithi, Lugha ya Kifasihi na Sarufi ........... 2

1.2 SEHEMU B: Utungaji ........................................................................ 59

1.3 SEHEMU C: Ufahamu ...................................................................... 65

2.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI ......................................................................... 75

3.0 HITIMISHO ........................................................................................ 77

4.0 MAPENDEKEZO ................................................................................ 78

KIAMBATISHO CHA PEKEE .................................................................... 80

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ya somo la Kiswahili katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2022. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa waliofanya mtihani huu kwa wanafunzi wanaosoma ngazi ya elimu ya msingi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla. Taarifa hii inaonesha umahiri walionao wanafunzi katika kujibu maswali na changamoto zilizowakabili. Aidha, taarifa inaonesha mahiri zilizojibiwa vizuri zaidi na zilizokuwa na changamoto na kutoa mapendekezo.

Katika taarifa hii mambo mbalimbali yaliyochangia watahiniwa kujibu vizuri maswali ya mtihani huu yamebainishwa. Mambo hayo ni pamoja na watahiniwa kuelewa matakwa ya swali na kuwa na maarifa ya kutosha katika mahiri za somo la Kiswahili zilizopimwa katika mtihani. Usahihi wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa ni ushahidi kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ulifanyika vizuri. Aidha, watahiniwa wachache walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuchagua jibu zaidi ya moja au kutochagua jibu lolote. Vilevile, watahiniwa wengine hawakuelewa maudhui ya ushairi na kushindwa kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umefanyika kwa kutumia maelezo, jedwali na vielelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho huu utakuwa chachu kwa wadau mbalimbali wa elimu katika kuchukua hatua stahiki ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2022 wa somo la Kiswahili ulifanyika tarehe 06 Oktoba, 2022. Jumla ya watahiniwa 1,384,186 walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2022 kwa somo la Kiswahili. Waliofanya mtihani walikuwa 1,347,979 sawa na asilimia 97.38. Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni 1,206,423, sawa na asilimia 89.50.

Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali arobaini na tano (45). Maswali arobaini (swali la 1-40) yalikuwa ya kuchagua jibu sahihi na kila swali lilikuwa na alama moja (1). Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu A, B, na C. Sehemu A ilihusu Kusikiliza Hadithi, Lugha ya Kifasihi, na Sarufi. Sehemu hiyo ilikuwa na alama thelathini na tano (35). Sehemu B ilihusu Utungaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kukamilisha kifungu cha maneno kwa kuchagua herufi iliyomo katika kisanduku na kujaza katika fomu ya OMR na ilikuwa na alama tano (5). Aidha, sehemu C ilihusu ufahamu ambapo mtahiniwa aliulizwa maswali mafupi matano (5) yaliyotokana na shairi alilopewa. Kila swali katika sehemu C lilikuwa na alama mbili (2).

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefanyika kwa maswali yote yaani maswali ya kuchagua herufi ya jibu sahihi na yale ya kujaza majibu mafupi. Uchambuzi umeonesha majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali kwa kuzingatia idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo katika swali la 1- 40. Aidha, kwa swali la 41- 45 uchambuzi umebainisha watahiniwa walioweza

kujibu kwa usahihi na walioshindwa pamoja na changamoto zilizowapata katika kujibu maswali husika.

Majibu ya watahiniwa yalifanyiwa uchambuzi kwa kutumia viwango vya ufaulu katika madaraja matatu yaliyokuwa na asilimia ya watahiniwa waliojibu swali husika kwa usahihi kama ifuatavyo: asilimia 60 - 100 ni daraja la kiwango kizuri cha ufaulu, 40 - 59 ni daraja la kiwango cha wastani cha ufaulu na 0 - 39 ni daraja la kiwango hafifu cha ufaulu.

Katika taarifa hii, chati na majedwali ya uchambuzi yametumika kuwasilisha takwimu za kiwango cha ufaulu wa watahiniwa. Katika majedwali na chati hizo, herufi ya jibu sahihi imeoneshwa kwa alama ya nyota (*). Aidha, takwimu za watahiniwa ambao ama walichagua jibu zaidi ya moja au hawakujibu swali, zimeoneshwa kwa kutumia neno "*Mengine*" katika majedwali na chati za uchambuzi. Vilevile, rangi ya kijani, njano na nyekundu kwenye chati na majedwali zinawakilisha kiwango kizuri, cha wastani na hafifu cha ufaulu, mtawalia.

## 1.1 SEHEMU A: Kusikiliza Hadithi, Lugha ya Kifasihi na Sarufi

Sehemu hii ilikuwa na maswali thelathini na tano (35). Maswali saba (1-7) yalipima umahiri mahususi wa kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. Aidha, katika swali la 1-5 mtahiniwa alitakiwa kusikiliza hadithi na kujibu maswali. Swali la nane (8) hadi (35) yalipima umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma. Watahiniwa walitakiwa kusikiliza hadithi ifuatayo; kisha kujibu maswali yanayofuata:

*Hapo zamani za kale Kuku na Mwewe waliishi pamoja mwituni. Walishirikiana kama ndugu waliotoka ukoo mmoja. Siku moja Mwewe alimuomba Kuku amlelee watoto wake. Yeye alipata safari ya mbali. Kuku alikubali kwa shingo upande kwa kuwa alikuwa na majukumu mengi.*

*Baada ya Mwewe kukaa mbali kwa muda mrefu kijijini palitokea janga la njaa kali. Kuku aliwasitiri watoto wake kwa kuwapa chakula na kuwaweka kando na watoto wa Mwewe. Watoto wa Mwewe walidhoofika na kuanza kufa mmoja baada ya mwingine.*

*Baada ya muda kupita, Mwewe alirejea kijijini na kukuta hali ya kustaajabisha. Alikuta watoto wake wote wamekufa. Uchungu kama mkuki mkali ulimchoma Mwewe moyoni mwake. Alikunja ndita na kujiuliza, imekuwaje watoto wangu wapoteze uhai? Au alishindwa kuwalea kwa sababu familia ilikuwa kubwa akazidiwa? Na kwa nini alikubali kwa ulimi wake kuwa atawalea wanangu?*

*Mwewe akaongea kwa hasira, "Mwosha, huoshwa". Kufumba na kufumbua Mwewe akanyakuwa kifaranga mmoja wa Kuku na kupaa naye angani. Kuku alipiga yowe kuomba msaada lakini ilishindikana kumpata Mwewe. Mpaka sasa bado kuna uadui mkubwa kati ya Kuku na Mwewe. Mwewe bado analipa kisasi kwa Kuku.*

Baada ya watahiniwa kusomewa hadithi mara mbili walitakiwa kujibu swali la 1-5 kwa lengo la kupima uelewa wao kuhusu hadithi waliyosikiliza. Maswali yalikuwa kama ifuatavyo:

**Swali la 1:** Hadithi uliyosomewa inahusu nini?

A Urafiki wa Kuku na ndege


B Uadui wa Kuku na Mwewe

C Urafiki wa Mwewe na vifaranga

D Watoto wa Kuku na Mwewe

E Undugu wa Kuku na Ndege

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuelewa hadithi aliyoisikiliza inahusu nini. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Chati Na. 1 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo:




**Chati Na**. *1: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa asilimia 85.68 sawa na watahiniwa 1,157,314 walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu B *Uadui wa Kuku na Mwewe*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha ya kusikiliza na kuelewa hadithi ipasavyo, hivyo kuelewa maudhui ya hadithi ambayo

ilihusu ugomvi wa Kuku na Mwewe. Ugomvi huo ulisababishwa na janga la njaa ambapo Kuku aliwasitiri watoto wake kwa kuwapa chakula na kuwaweka kando watoto wa Mwewe; hatimaye walidhoofika na kufa wote.

Hata hivyo, watahiniwa 185,706 sawa na asilimia 13.75 walichagua kati ya vipotoshi *A Urafiki wa kuku na ndege,* C *Urafiki wa Mwewe na vifaranga,* D *Watoto wa Kuku na Mwewe na* E *Undugu wa Kuku na Ndege.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *urafiki wa Kuku na Ndege* walishindwa kubaini kuwa, mhusika ndege hakutajwa katika hadithi na wala hakuelezwa kuwa na uhusiano na Kuku au Mwewe. Vilevile, waliochagua kipotoshi C *urafiki wa Mwewe na vifaranga* walishindwa kuelewa kuwa katika hadithi waliyosomewa Mwewe na vifaranga hawakuwa na mahusiano kwani vifaranga walikuwa ni watoto wa Kuku. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi *watoto wa Kuku na Mwewe* haukuwa sahihi kwani watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa hapakuwa na uhusiano wowote kati ya wahusika hao kwani Kuku alikuwa na uhusiano na vifaranga vyake na Mwewe alikuwa na uhusiano na watoto wake tu. Pia, uteuzi wa kipotoshi *undugu wa Kuku na Ndege* haukuwa sahihi kwa kuwa ndege hakutajwa katika hadithi. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kusikiliza na kuelewa hadithi waliyosomewa.

**Swali la 2:** Kwa nini Kuku alikubali kuwalea watoto wa Mwewe kwa shingo upande?

A Alikuwa hampendi Mwewe


B Alikuwa na majukumu mengi

C Kwa sababu kulikuwa na njaa

D Kwa sababu Kuku alikuwa mchoyo

E Kwa sababu Mwewe alikuwa na hasira

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha sababu zilizomfanya Kuku kukubali kuwalea watoto wa Mwewe kwa shingo upande. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Chati Na. 2 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa watahiniwa 1,109,881 sawa na asilimia 82.17 walichagua jibu sahihi *B alikuwa na majukumu mengi.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri, maarifa na weledi wa kutosha katika kusikiliza na kuelewa maudhui ya hadithi waliyosomewa na msimamizi. Hivyo, kuweza kutambua kuwa Kuku alikubali kwa shingo upande kuwalea watoto wa Mwewe kwa kuwa alikuwa na majukuimu mengi.

Hata hivyo, asilimia 17.28 sawa na watahiniwa 233,502 walichagua kati ya vipotoshi *A Alikuwa hampendi Mwewe, C Kwa sababu kulikuwa na*

*njaa, D Kwa sababu kuku alikuwa mchoyo, E Kwa sababu Mwewe alikuwa na hasira.* Uchaguzi wa kipotoshi *alikuwa hampendi Mwewe* haukuwa sahihi kwa sababu kabla ya kuwa maadui Kuku na Mwewe walishirikiana kama ndugu. Vilevile, uchaguzi wa kipotoshi *kwa sababu kulikuwa na njaa* haukuwa sahihi kwa kuwa janga la njaa lilitokea baada ya Mwewe kuondoka na siyo wakati Kuku alipokuwa anakabidhiwa jukumu la kulea watoto wa Mwewe. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *kwa sababu Kuku alikuwa mchoyo* siyo sahihi kwani Kuku alionesha hali ya kuzidiwa na majukumu. Vilevile, waliochagua kipotoshi *kwa sababu Mwewe alikuwa na hasira* walishindwa kuelewa kuwa Mwewe hakuwa na hasira wakati wa kumkabidhi Kuku watoto wake bali alipata hasira mara baada ya kukuta watoto wake wote wamekufa. Kwa ujumla uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi hivyo kushindwa kubainisha sababu ya Kuku kukubali kuwalea watoto wa Mwewe kwa shingo upande.

**Swali la 3:** Mwewe aliporejea kutoka safarini alikutana na jambo lipi la kustaajabisha?

A Kifo cha watoto wake

B Kifo cha mtoto wake mmoja


C Afya bora ya watoto wa Kuku

D Watoto wake wote kuwa na njaa

E Kifo cha watoto wa Kuku

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha jambo la kustaajabisha ambalo Mwewe alikutana nalo wakati akirejea kutoka safarini. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Chati

Na. 3 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa watahiniwa 1,220,910 sawa na asilimia 90.39 walichagua jibu sahihi A *Kifo cha watoto wake*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza hadithi na kuelewa maudhui yaliyomo. Hivyo, waliweza kubaini kuwa Mwewe aliporejea kutoka safarini alikuta watototo wake wamekufa.

Hata hivyo, watahiniwa 122,957 sawa na asilimia 9.10 walichagua kati ya vipotoshi *B Kifo cha mtoto wake mmoja*, *C Afya bora ya watoto wa Kuku, D Watoto wake wote kuwa na njaa*, na E *Kifo cha watoto wa Kuku*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kifo cha mtoto wake mmoja* walishindwa kuelewa kuwa Mwewe alikuwa na watoto zaidi ya mmoja katika habari husika na wote walikufa. Vilevile, waliochagua kipotoshi

*afya bora ya watoto wa Kuku* walishindwa kuelewa kuwa kilichomshtusha Mwewe ni kifo cha watoto wake na siyo afya bora ya watoto wa Kuku. Pia, katika hadithi hali ya afya ya watoto wa kuku haikubainishwa bayana. Vilevile, waliochagua kipotoshi *watoto wake wote walikuwa na njaa* hawakuelewa kuwa wakati wa njaa mwewe hakuwepo hivyo siyo sababu ya msingi iliyomfanya Mwewe kustaajabu, ingawa kifo cha watoto wake wote kilitokana na njaa. Aidha, waliochagua kipotoshi *kifo cha watoto wa Kuku,* hawakuelewa kuwa waliokufa ni watoto wa Mwewe na siyo watoto wa Kuku. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao walikosa umahiri wa kusikiliza na kubaini maudhui yaliyokuwa katika hadithi husika.

**Swali la 4:** Sababu gani ilimfanya Mwewe kumuomba Kuku amlelee watoto wake?

A Kuku alikuwa mkarimu


B Kuku alipenda watoto wa Mwewe

C Waliishi pamoja mwituni

D Alipata safari ya mbali

E Walishirikiana kama ndugu

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe sababu zilizomfanya Mwewe kumuomba Kuku amlelee Watoto wake. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Chati Na. 4 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 4:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa watahiniwa 1,091,521 sawa na asilimia 80.81 walichagua jibu sahihi *D alipata safari ya mbali* ambayo ni sababu iliyomfanya Mwewe kumuomba Kuku amlelee watoto wake*. Jambo* linaloonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha hivyo kuweza kusikiliza hadithi na kuelewa maudhui.


Hata hivyo, asilimia 19.04 sawa na watahiniwa 251,193 walichagua kati ya vipotoshi *A Kuku alikuwa mkarimu; B Kuku alipenda watoto wa Mwewe;* C *Waliishi pamoja mwituni;* na E *Walishirikiana kama ndugu.* Uchaguzi wa kipotoshi *Kuku alikuwa mkarimu* haukuwa sahihi kwa sababu Kuku aliwasitiri watoto wake kwa kuwapa chakula na kuwaweka kando watoto wa Mwewe. Waliochagua kipotoshi *Kuku alipenda watoto wa Mwewe* hawakuwa sahihi kwa kuwa kuku alitumia muda mwingi kuangalia watoto wake na kuacha watoto wa mwewe kudhoofika hadi kufa mmoja baada ya mwingine. Vilevile, waliochagua kipotoshi *kuishi pamoja mwituni* walishindwa kuelewa kuwa Kuku na Mwewe ni ndege

ambao huishi mwituni ila sio sababu iliyomfanya Mwewe kumuomba Kuku amlelee watoto wake. Aidha, waliochagua kipotoshi *kushirikiana kama ndugu* hawakuelewa kuwa ushirikiano huo wa Kuku na Mwewe ulikuwa sio sababu ya Kuku kuombwa na Mwewe amlelee watoto wake kwa sababu ushirikiano huo ulijengwa kwa kuwa wote ni ndege wanaoishi pamoja mwituni. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kusikiliza na kuonesha uelewa wa hadithi waliyosomewa na msimamizi.

**Swali la 5:** Katika kijiji walichoishi Kuku na Mwewe kulitokea janga gani?

A Njaa kali
B Uchoyo
C Vifo
D Uadui wa Kuku na Mwewe
E Usaliti

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe janga lililotokea katika Kijiji walichoishi Kuku na Mwewe. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Chati Na. 5 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 5:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa watahiniwa 1,168,058 sawa na asilimia 86.47 walichagua jibu sahihi *A Njaa kali*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha ya kusikiliza hadithi waliyosomewa; hivyo kuelewa vyema maudhui yaliyomo ambapo waliweza kutambua janga lililotokea katika kijiji walichoishi Kuku na Mwewe.


Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 175,184 sawa na asilimia 12.97 walichagua kati ya vipotoshi *B Uchoyo, C Vifo, D Uadui wa Kuku na Mwewe, na E Usalitii.* Uchaguzi wa kipotoshi *uchoyo,* ulitokana na watahiniwa kuhusianisha na tabia ya Kuku ya kuwanyima watoto wa mwewe chakula japo ni kinyume na matakwa ya swali. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *vifo* walishindwa kuelewa kuwa vifo vilivyotokea vilikuwa vya watoto wa Mwewe pekee na siyo kijiji chote. Aidha, waliochagua kipotoshi *Uadui wa Kuku na Mwewe* hawakuelewa kwamba hali hiyo ilitokea baada ya kuku kughairi kuwapa watoto wa Mwewe chakula; hatimaye kufa kwa njaa na wala uadui huo haukuwa

janga la Kijiji kizima. Vilevile, waliochagua kipotoshi *usaliti* walihusisha na kitendo cha Kuku kuwasitiri watoto wake kwa chakula na kuwatenga watoto wa Mwewe ambapo hili sio janga lililozungumziwa katika hadithi. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kusikiliza na kuelewa hadithi waliyoisikiliza.

**Swali la 6:** “Bibi anaosha vyombo.” Kauli ya kutendwa ya sentensi hii ni ipi kati ya zifuatazo?

A Vyombo vinaosheka na bibi
B Bibi anaosheana vyombo.
C Vyombo vinaoshwa na bibi
D Bibi anaoshewa vyombo
E Vyombo vinaoshewa na bibi

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuelewa kauli ya kutendwa katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 6 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 6:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa watahiniwa 996,131 sawa na asilimia 73.74 walijibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua *C Vyombo vinaoshwa na bibi.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika kutumia kauli mbalimbali za vitenzi na kubaini kuwa, kauli ya kutendwa huoneshwa na kiambishi **-w-** inayotokea baada ya mzizi na kabla ya kiambishi tamati maana.


Hata hivyo, asilimia 25.52 sawa na watahiniwa 344,596 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao walichagua kati ya vipotoshi A *Vyombo vinaosheka na bibi, B Bibi anaosheana vyombo*, *D Bibi anaoshewa vyombo,* na *E Vyombo vinaoshewa na bibi*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Vyombo vinaosheka na bibi* hawakuelewa kuwa, "osheka" ni kauli ya kutendeka yenye kiambishi **-ek-** katika kitenzi *osha*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Bibi anaosheana vyombo* walishindwa kuelewa kuwa "osheana" ni kauli ya kutendeana yenye kiambishi **-ean-** katika kitenzi *osha*. Vilevile, waliochagua kipotoshi *Bibi*

*anaoshewa vyombo,* hawakuelewa kuwa “oshewa” ni kauli ya kutendewa yenye kiambishi **-ew-** katika kitenzi hicho. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *Vyombo vinaoshewa na bibi* walishindwa kuelewa nomino “vyombo” haiwezi kutenda bali kutendwa/kutendewa (kosa la kimantiki). Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao kutokuwa na umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali hususani katika kali ya kutendwa.

**Swali la 7:** Hapo ________ alipojificha yule mwizi. Neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A ndimo
B ndiko
C ndipo
D ndio
E ndiyo

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 7 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa watahiniwa 1,055,927 sawa na asilimia 78.11 walijibu vizuri swali hili kwa kuchagua jibu sahihi *C ndipo*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika kuandika sentensi zenye kuonesha mahali, watu au vitu vilipo. Aidha, waliweza kubaini kuwa neno "ndipo" ni kitenzi kishirikishi hivyo, hutoa maana iliyokamili katika swali husika.

Hata hivyo, watahiniwa 284,522 sawa na asilimia 21.07 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua kati ya vipotoshi A *ndimo* B *ndiko* D *ndio, na E ndiyo*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndimo* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya kuwa ndani ya kitu. Uchaguzi wa kipotoshi *ndiko* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo linatumika kuonesha umbali wa kitu. Vilevile, waliochagua kipotoshi *ndio* hawakuelewa kuwa neno hilo hutumika kuonesha kitenzi kishirikishi kwa binadamu na wanyama. Kadhalika, waliochagua kipotoshi *ndiyo* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo linatumika katika kukubali jambo.

Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia upatanisho wa kisarufi katika sentensi za lugha ya Kiswahili.

Swali la 8 hadi 19 yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali,* hususan umahiri mahususi wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 8:** Neno lipi ni jumuishi kwa maneno haya “mshale, panga, kisu, upinde?”

A Zana


B Nyenzo

C Vyuma

D Pembejeo

E Nyara

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia msamiati katika kuwasiliana. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 8 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 8:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa watahiniwa 1,109,726 sawa na asilimia 82.15 walijibu vizuri swali. Watahiniwa hao walichagua jibu sahihi *A Zana* ambalo lina maana ya chombo au kifaa kinachohitajika kufanyia kazi fulani. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kujua misamiati mbalimbali inayoundwa kutokana na maneno jumuishi.

Hata hivyo, watahiniwa 230,711 sawa na asilimia 17.08 walichagua kati ya vipotoshi B *Nyenzo*, C *Vyuma, D Pembejeo* na E *Nyara*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nyenzo* hawakubaini kuwa maana ya neno hilo ni vitu vinavyotumika kuinulia au kubiringisha kitu kingine ili kurahisisha kazi. Uchaguzi wa kipotoshi *vyuma* ulitokana na kushindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya madini magumu yanayotumiwa kujengea na kuundia vitu. Vilevile, walishindwa kubaini kuwa neno upinde ni kifaa ambacho hakitokani na madini ya chuma. Sambamba na hayo, uteuzi wa kipotoshi *pembejeo* ulitokana na kutokuelewa kuwa neno hilo hujumuisha *mbegu, dawa na mbolea* kwa ajili ya kilimo. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *nyara*, haukuzingatia muktadha wa matumizi ya neno hilo

lenye maana ya mali rasmi yenye matumizi ya Serikali pekee. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia msamiati mbalimbali inayoundwa na maneno jumuishi.

**Swali la 9:** “Sikutegemea kama Ndoni ni kichwa maji kiasi hiki.” Je Ndoni alikuwa ni mtu mwenye hali gani ?

A Ujanja


B Kutokuwa msikivu

C Ujinga

D Ukorofi

E Upole

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana za nahau katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 9 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 9**: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa watahiniwa 757,621 sawa na asilimia 56.09 walichagua jibu sahihi C *ujinga.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya nahau “kichwa maji” kuwa ni mtu mjinga asiyeelewa hata akielekezwa.

Hata hivyo, watahiniwa 578,788 sawa na asilimia 42.85 walichagua kati ya vipotoshi A *Ujanja*, B *Kutokuwa msikivu,* D *Ukorofi* na E *Upole*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ujanja* walishindwa kuelewa kuwa ujanja ni hila au udanganyifu*.* Uteuzi wa kipotoshi *kutokuwa msikivu* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa nahau hiyo haina uhusiano na uelekevu/utiifu. Aidha, waliochagua kipotoshi *ukorofi* walishindwa kuelewa kuwa kina maana ya usumbufu ambapo ni kinyume na maana stahiki ya nahau husika*.* Pia, uteuzi wa kipotoshi *upole* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya utulivu na utaratibu kinyume na maana ya nahau hiyo.

Uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa mahiri katika kutumia nahau na maana zake katika tungo za kifasihi.

**Swali la 10:** "Akitokea watu wote humuona." Jibu la kitendawili hiki ni lipi ?

A Radi


B Mwezi

C Nyota

D Jua

E Upinde wa mvua

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutega na kutegua vitendawili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 10 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 10**: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*


Chati Na. 10 inaonesha kuwa watahiniwa 890,802 sawa na asilimia 65.95 walichagua jibu sahihi D *Jua*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutegua kitendawili hivyo kuweza kuelewa kuwa jua hutoa mwanga mkali na joto ambalo kila mtu analiona au kuhisi litokeapo.

Hata hivyo, watahiniwa 444,737 sawa na asilimia 32.92 walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi. Watahiniwa hao walichagua kati ya vipotoshi A *radi*, B *mwezi*, C *nyota* na E *upinde wa mvua*. Uchaguzi wa vipotoshi *radi*, *mwezi, nyota,* na *upinde wa mvua* ulitokana na kutokuelewa kuwa muonekano wa vitu hivyo katika anga si dhahiri kwa watu wote kwa wakati mmoja kuviona bali huweza kuonekana na wakati mwingine visionekane kabisa kwa kumezwa na mwanga wa jua. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha bayana kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutega na kutegua vitendawili mbalimbali vya Kiswahili.

**Swali la 11:** “Mwarabu wangu mkali hana panga wala kisu”. Jibu la kitendawili hiki ni lipi kati ya yafuatayo?

A Moto
B Jua
C Mvuke
D Pasi
E Jiko

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutega na kutegua vitendawili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 11 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 11*: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo***

Chati Na. 11 inaonesha kuwa watahiniwa 972,418 sawa na asilimia 71.99 walijibu vizuri swali hili kwa kuchagua A *Moto.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutega na kutegua vitendawili.

Hata hivyo, watahiniwa 362,778 sawa na asilimia 26.86 walichagua kati ya vipotoshi B *jua,* C *mvuke,* D *pasi* na E *jiko.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *jua, mvuke, pasi* na *jiko* walishawishika kutokana na madhara ya vitu hivyo kwa binadamu ambapo walihusianisha na muktadha wa kitendawili husika ambapo huelezea ukali. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutega na kutegua vitendawili katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 12:** Teketeke huzaa gumugumu, gumugumu huzaa teketeke. Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Mgomba


B Mpapai

C Mfenesi

D Mchungwa

E Mhindi

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima. umahiri wa mtahiniwa wa kutega na kutegua vitendawili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 12 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 12:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa watahiniwa 823,920 sawa na asilimia 61.00 walichagua jibu sahihi E *mhindi.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mfumo wa uzazi wa mahindi ulivyoakisi

umbo la kitendawili hicho. Watahiniwa hao walifahamu kuwa kabla mbegu za mahindi hazijakomaa huwa teketeke na zinapandwa zikiwa ngumu.

Hata hivyo, watahiniwa 510,763 81 sawa na asilimia 37 walichagua kati ya vipotoshi A *mgomba,* B *mpapai,* C *mfenesi,* na D *mchungwa.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *mgomba*, *mpapai*, *mfenesi,* na *mchungwa* walishindwa kuelewa kuwa mimea hiyo hupandikizwa kama miche ambayo huzaa matunda yasiyo magumu na yanayotakiwa kutumika kwa muda maalum ili yasiharibike kinyume na mhindi unaopandwa kama mbegu ngumu. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutega na kutegua vitendawili husika.

**Swali la 13:** "Ando alijipalia makaa baada ya kuwatukana maaskari." Neno **kujipalia makaa** lina maana gani?

A Kujihami


B Kujihukumu

C Kujidhalilisha

D Kukimbia mwenyewe

E Kujitia matatani

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutumia nahau na kuelezea maana zake. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 13 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 13:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa watahiniwa 775,013 sawa na asilimia 57.38 walichagua jibu sahihi E *kujitia matatani*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya matumizi ya nahau na maana zake katika miktadha mbalimbali.

Hata hivyo, watahiniwa 560,038 sawa na asilimia 41.46 walichagua kati ya vipotoshi A *kujihami*, B *kujihukumu*, C *kujidhalilisha* na D *kukimbia mwenyewe*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kujihami* walishindwa kuelewa kuwa hiki ni kitendo cha kujilinda usipate matatizo kinyume na kujipalia makaa. Waliochagua kipotoshi *kujihukumu*, hawakuelewa kuwa neno hilo lina maana ya kujipa adhabu. Aidha, kipotoshi *kujidhalilisha* ni neno lenye maana ya kujivunjia heshima au kuwa duni. Pia, kipotoshi, *kukimbia mwenyewe* hawakuelewa kuwa maneno hayo yana maana ya mtu husika kwenda kwa haraka sana kwa kutumia vidole zaidi kuliko visigino. Hivyo, kutokana na maana ya maneno hayo kutokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na nahau husika, inaonesha kuwa

watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia na kuelewa maana husika.

**Swali la 14:** **“**Vijana wenye nia mbaya walitimba mali za serikali.” Je, nahau “timba mali” kama ilivyotumika katika sentensi hii ina maana ipi?

A Kuongeza mali
B Kutumia mali ovyo
C Kupoteza mali
D Kuharibu mali
E Kuuza mali

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutumia nahau katika sentensi na kuelezea maana zake. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 1 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 60,696 | 670,317 | 93,936 | 379,393 | 130,824 | 15,614 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 4.49 | 49.62 | 6.95 | 28.09 | 9.69 | 1.16 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa watahiniwa 670,317 sawa na asilimia 49.62 walichagua jibu sahihi B *kutumia mali ovyo.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya nahau; hivyo kuelewa maana ya nahau “timba mali” kuwa ni kutumia mali bila kuwa na uchungu nayo.

Hata hivyo, watahiniwa 664,849 sawa na asilimia 49.22 walichagua kati ya vipotoshi A *kuongeza mali* C *kupoteza mali, D kuharibu mali,* na E

*kuuza mali*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kuongeza mali* walishindwa kuelewa kuwa nahau hiyo haina maana ya kuongeza mali bali ni kutumia mali ovyo. Waliochagua kipotoshi *kupoteza mali* hawakuelewa kuwa hiki ni kitendo cha kuondokewa na baadhi ya vitu katika mali walizonazo; hivyo ni kinyume na matakwa ya swali. Pia, waliochagua kipotoshi *kuharibu mali* hawakuelewa kuwa ni kitendo cha kuifanya mali isiwe na manufaa tena. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *kuuza mali* walishindwa kuelewa kuwa ni kitendo cha kufanya biashara na kujipatia faida; hivyo haihusiani na maana ya nahau "timba mali". Kwa ujumla watahiniwa hao walikosa umahiri wa kutumia nahau katika sentensi na kueleza maana zake.

**Swali la 15:** "Mama hupenda kusafiri kila mwezi." Sentensi hii ipo katika hali gani kati ya zifuatazo ?

A Kawaida
B Mazoea
C Kuendelea
D Kutendeka
E Timilifu

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia nyakati mbalimbali katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 2 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 77,026 | 967,032 | 130,619 | 76,963 | 90,005 | 9,135 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 5.70 | 71.59 | 9.67 | 5.70 | 6.66 | 0.68 |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa watahiniwa 967,032 sawa na asilimia 71.59 walichagua jibu sahihi B *mazoea.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu hali mbalimbali za vitenzi katika sentensi. Hivyo, waliweza kubaini kuwa kiambishi **hu-** katika kitenzi huelezea tendo linavyofanyika mara kwa mara yaani kwa mazoea.

Hata hivyo, watahiniwa 374,613 sawa na asilimia 27.73 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua kati ya vipotoshi A *kawaida*, C *kuendelea*, D *kutendeka na* E *timilifu*. Uteuzi wa kipotoshi *kawaida* ulitokana na watahiniwa kukosa maarifa katika kubaini hali za matendo ambapo kiuhalisia hakuna hali ya kawaida katika lugha ya Kiswahili. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi *kuendelea,* watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa, hali hiyo hudhihirika katika sentensi kwa matumizi ya kiambishi njeo *-na-* katika kitenzi. Watahiniwa walichagua kipotoshi *kutendeka,* walishindwa kuelewa kuwa hiyo ni kauli na sio hali ambapo huonesha kauli ya kutendeka inayoundwa na kiambishi -ek- katika kitenzi. Pia, uteuzi wa kipotoshi *timilifu* walishindwa kuelewa kuwa hali timilifu hutumia kiambishi *-me-* katika kuelezea tendo. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutumia hali mbalimbali za matendo katika sentensi.

**Swali la 16:** “Juzi tulicheza ngoma usiku kucha.” Kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi ni kipi kati ya vifuatavyo ?

A tu-

B -li-

C -chez-

D -a

E -za

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia nafsi mbalimbali katika hali ya umoja na wingi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 3 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 840,488 | 174,331 | 230,318 | 60,125 | 34,702 | 10,816 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 62.22 | 12.91 | 17.05 | 4.45 | 2.57 | 0.80 |

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa watahiniwa 840,488 sawa na asilimia 62.22 walichagua jibu sahihi A *tu-.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya nafsi mbalimbali. Kadhalika, waliweza kubaini kuwa nafsi ya kwanza wingi ni **sisi** ambapo kiambishi chake ambacho hutokea katika kitenzi ni **tu-**.

Hata hivyo, watahiniwa 499,476 sawa na asilimia 36.98 walichagua kati ya vipotoshi B *-li-*, C *–chez-*, D *-a na* E *-za*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *-li-* walishindwa kuelewa kuwa kiambishi hicho huonesha wakati uliopita. Pia, waliochagua kipotoshi *-chez-* walishindwa kuelewa kuwa ni mzizi wa neno. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *-a* walishindwa kuelewa kuwa hicho ni kiambishi tamati kinachokamilisha maana katika neno. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *-za* ulitokana na kukosa uelewa wa maumbo mbalimbali ya vitenzi kwa kuwa hiyo ni silabi ya nne katika neno *tulicheza* yaani {**tu**} {**li**} {**che**} {**za**}. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kuelewa matumizi ya nafsi mbalimbali katika vitenzi.

**Swali la 17:** “Mimi niliunda kanuni za lugha ya Kiswahili.” Sentensi hii ikikanushwa itakuwa ipi kati ya zifuatazo?

A Mimi sitaunda kanuni za lugha ya Kiswahili.

B Mimi sijaunda kanuni za lugha ya Kiswahili.

C Mimi sikuunda kanuni za lugha ya Kiswahili.

D Mimi nimeunda kanuni za lugha ya Kiswahili.

E Mimi ningeunda kanuni za lugha ya Kiswahili.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima dhana ya ukanushi katika nyakati mbalimbali katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 4 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 156,950 | 213,382 | 749,950 | 173,012 | 45,349 | 12,137 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 11.62 | 15.80 | 55.52 | 12.81 | 3.36 | 0.90 |

Jedwali Na. 4 linaonesha kuwa watahiniwa 749,950 sawa na asilimia 55.52 walichagua jibu sahihi C *Mimi sikuunda kanuni za Lugha ya Kiswahili*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya ukanushi katika wakati uliopita ambapo waliweza kuelewa kuwa ukanushi katika wakati uliopita huhusisha na kiambishi –ku- katika kitenzi kulingana na muktadha wa sentensi husika.

Hata hivyo, watahiniwa 588,693 sawa na asilimia 43.58 walichagua kati ya vipotoshi A *Mimi sitaunda kanuni za lugha ya Kiswahili*; B *Mimi sijaunda kanuni za lugha ya Kiswahili*; D *Mimi nimeunda kanuni za lugha*

*ya Kiswahili,* na E *Mimi ningeunda kanuni za lugha ya Kiswahili*. Uteuzi wa kipotoshi *Mimi sitaunda kanuni za lugha ya Kiswahili*, watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa sentensi hiyo hudokeza ukanushi wakati ujao. Pia, waliochagua kipotoshi *Mimi sijaunda kanuni za lugha ya Kiswahili* walishindwa kuelewa kuwa sentensi hiyo hudokeza ukanushi wa sentensi katika wakati timilifu. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *Mimi nimeunda kanuni za lugha ya Kiswahili* walishindwa kuelewa kuwa sentensi hii haidokezi ukanushi bali uyakinifu kinyume na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *Mimi ningeunda kanuni za lugha ya Kiswahili*, walishindwa kuelewa kuwa sentensi hii haidokezi ukanushi. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutumia ukanushi wa matukio katika nyakati mbalimbali.

**Swali la 18:** "Ingawa walipata vikwazo vingi njiani, hatimaye walifika salama. Sentensi hii iko katika wakati gani kati ya nyakati zifuatazo?

A Ujao
B Uliopita
C Uliopo
D Mazoea
E Timilifu

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kujua nyakati mbalimbali katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 5 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 55,086 | 1,059,649 | 120,802 | 42,638 | 63,146 | 9,459 |
| Asilimia ya watahiniwa | 4.08 | 78.45 | 8.94 | 3.16 | 4.67 | 0.70 |

Jedwali Na. 5 linaonesha kuwa watahiniwa 1,059,649 sawa na asilimia 78.45 walichagua jibu sahihi B, *uliopita.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubainisha nyakati katika sentensi ambapo walieleza kuwa kiambishi **-li-** katika vitenzi "walipata" na "walifika" vilivyopo katika swali husika vikionesha wakati uliopita.

Hata hivyo, watahiniwa 281,672 sawa na asilimia 20.85 walishindwa kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua kati ya vipotoshi A *ujao,* C *uliopo*, D *mazoea* na E *timilifu*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ujao* hawakuwa sahihi kwa kuwa wakati ujao hubainishwa kwa kutumia kiambishi ***-ta-*** katika kitenzi. Pia, waliochagua kipotoshi *uliopo* hawakuelewa kuwa njeo hiyo hubainishwa kwa kiambishi ***-na-*** katika kitenzi. Aidha, waliochagua kipotoshi *mazoea,* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni hali na siyo wakati. Aidha, waliochagua kipotoshi *timilifu* walishindwa kuelewa kuwa wakati timilifu huundwa na kiambishi njeo ***-me-*** katika kitenzi. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kubainisha viambishi vya njeo ya wakati liopita -li- katika sentensi husika.

**Swali la 19:** Yeye alisema "siwezi kuja kwenu." Kauli taarifa ya sentensi hii ni ipi kati ya zifuatazo?

A Yeye alisema kwamba haji kwenu.

B Yeye alisema kwamba sitakuja kwetu.

C Yeye alisema hataweza kuja kwenu.

D Yeye alisema kuwa hawezi kuja kwenu.

E  Yeye alisema kwamba hawezi kuja kwetu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutunga sentensi kwa kutumia kauli taarifa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Jedwali Na. 6 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 124,891 | 116,543 | 218,829 | 475,262 | 400,100 | 15,155 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 9.25 | 8.63 | 16.20 | 35.18 | 29.62 | 1.12 |

Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa watahiniwa 935,525 sawa na asilimia 69.26 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao walichagua kati ya vipotoshi A *Yeye alisema kwamba haji kwenu*, B *Yeye alisema kwamba sitakuja kwetu*, C, *Yeye alisema hataweza kuja kwenu* na D, *Yeye alisema kuwa hawezi kuja kwenu*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Yeye alisema kwamba haji kwenu* walishindwa kutambua kuwa sentensi hiyo imezingatia zaidi ukanushi badala ya kauli taarifa ya sentensi iliyotolewa. Vilevile, waliochagua kipotoshi *Yeye alisema kwamba sitakuja kwetu* hawakuwa sahihi kwa kuwa kauli hiyo imezingatia wakati ujao badala ya wakati uliopita. Waliochagua kipotoshi *Yeye alisema hataweza kuja kwenu* hawakutambua kuwa sentensi hii ipo katika hali ya ukanushi wakati ujao badala ya wakati uliopita. Pia watahiniwa waliochagua kipotoshi *Yeye alisema kuwa hawezi kuja kwenu* hawakujua kuwa kiwakilishi kimilikishi *kwenu* hakiendani na mpokea ujumbe. Kwa ujumla uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha

kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutunga sentensi kwa kutumia kauli taarifa.

Hata hivyo, watahiniwa 400,100 sawa na asilimia 29.62 walichagua jibu sahihi E *Yeye alisema kwamba hawezi kuja kwetu.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kutunga sentensi kwa kutumia kauli taarifa. Aidha, waliweza kubaini kuwa kauli taarifa ni kauli inayotolewa maelekezo yaliyosemwa awali kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji na maneno huweza hubadilika ila ujumbe unabaki ule ule.

Swali la 20 hadi 25 yaliandaliwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali*, katika umahiri mahususi wa kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.

**Swali la 20:** Katika neno "anaimba," kipi ni kiambishi tamati kati ya vifuatavyo?

A -na-
B -imb-
C -a
D -mba-
E -ba

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kueleza dhima mbalimbali za viambishi katika vitenzi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 7 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 7: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 180,735 | 385,742 | 550,965 | 163,602 | 56,457 | 13,279 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 13.38 | 28.56 | 40.79 | 12.11 | 4.18 | 0.98 |

Jedwali Na. 7 linaonesha kuwa watahiniwa 550,965 sawa na asilimia 40.79 walichagua jibu sahihi C (*-a).* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu dhima za viambishi mbalimbali katika vitenzi, hivyo kubainisha kwa usahihi kiambishi tamati katika neno "anaimba."

Hata hivyo, watahiniwa 799,815 sawa na asilimia 58.23 walichagua kati ya vipotoshi A *-na-*, B *-imb-*, D *-mba-* na E *-ba*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *-na-* walishindwa kuelewa kuwa kiambishi hicho kinadokeza njeo ya wakati uliopo. Aidha, uteuzi wa kipotoshi -imb-ulitokana na kukosa maarifa kuhusu mzizi wa neno. Hivyo hivyo, kipotoshi *-mba-* kilitokana na watahiniwa kukosa uelewa wa muundo wa silabi katika neno kwani umbo hilo ni silabi ya nne katika neno anaimba yaani {**a**} {**na**} {**i**} {**mba**}. Pia, waliochagua kipotoshi *-ba*, walishindwa kuelewa kuwa umbo hilo halina maana yoyote ya kisarufi. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo; hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu dhima ya viambishi mbalimbali katika vitenzi.

**Swali la 21: "**Baba alikuwa anakula ugali jana jioni." Katika sentensi hii neno lipi kati ya yafuatayo limetumika kama kitenzi kisaidizi katika sentensi?

A anakula

B baba

C alikuwa

D jana

E jioni

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kubainisha aina za maneno katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 8 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 292,736 | 90,208 | 722,444 | 137,528 | 93,825 | 14,039 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 21.67 | 6.68 | 53.48 | 10.18 | 6.95 | 1.04 |

Jedwali Na. 8 linaonesha kuwa watahiniwa 722,444 sawa na asilimia 53.48 walijibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao walichagua jibu C *alikuwa* kwa kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini matumizi sahihi ya aina za maneno katika sentensi. Hivyo, waliweza kubaini kuwa neno *alikuwa* kuwa ni kitenzi kisaidizi kwa sababu haliwezi kukamilisha sentensi kwa kutoa maana iliyokusudiwa bali huhitajika kitenzi kikuu kukamilisha maana katika sentensi husika ambacho ni *anakula*.

Hata hivyo, watahiniwa 614,297 sawa na asilimia 45.48 walichagua kati ya vipotoshi A *anakula*, B *baba,* D *jana* na E jioni. Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *anakula* hawakubaini kuwa neno hilo ni kitenzi kikuu. Vilevile, uchaguzi wa kipotoshi *baba,* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo limetumika kama nomino katika sentensi husika. Aidha, uteuzi wa vipotoshi *jana* na *jioni* vimetokana na kukosa uelewa kuwa maneno hayo ni vielezi. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa

watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi sahihi ya vitenzi, hivyo kushindwa kubainisha kitenzi kisaidizi.

**Swali la 22:** Mwalimu alikwenda kijijini kwao kuhani msiba. Katika sentensi hii neno lipi kati ya yafuatayo linaonesha hali ya umiliki?

A kijijini

B msiba

C kwao

D kuhani

E mwalimu

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu aina za maneno katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 9 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 122,082 | 149,309 | 804,105 | 166,809 | 94,581 | 13,894 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 9.04 | 11.05 | 59.53 | 12.35 | 7.00 | 1.03 |

Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa watahiniwa 804,105 sawa na asilimia 59.53 walichagua jibu sahihi C *kwao.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia maneno yanayoonesha umiliki wa mahali wa mtenda katika sentensi.

Hata hivyo, watahiniwa 532,781 sawa na asilimia 39.44 walichagua kati ya vipotoshi A *kijijini*, B *msiba*, D *kuhani,* na E *mwalimu.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kijijini* hawakuelewa kuwa neno hilo ni kielezi kinachoonesha mahali. Pia, waliochagua kipotoshi *msiba* hawakuelewa kuwa neno hili ni nomino. Vilevile, waliochagua kipotoshi *kuhani* hawakuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi. Aidha, waliochagua kipotoshi *mwalimu* hawakuelewa kuwa neno hilo ni nomino inayoonesha mtenda katika sentensi husika. Kwa ujumla, maneno hayo hayaoneshi umiliki wowote katika sentensi. Hivyo, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutumia maneno yanayoonesha umiliki katika sentensi waliyopewa.

**Swali la 23:** Mpangilio sahihi wa maneno “Anapenda kula mtoto wangu chakula” katika kuunda sentensi ni upi kati ya mipangilio ifuatayo?

A Mtoto wangu anapenda kula chakula


B Anapenda kula chakula mtoto wangu

C Mtoto wangu chakula anapenda kula

D Anapenda mtoto wangu kula chakula

E Wangu mtoto anapenda chakula kula

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuelewa mpangilio sahihi wa maneno katika kuunda sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Chati Na. 14 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 14**: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa watahiniwa 1,168,434 sawa na asilimia 86.50 walichagua jibu sahihi A *Mtoto wangu anapenda kula chakula.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kufahamu mpangilio sahihi wa maneno katika kuunda sentensi. Aidha, watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa sentensi hiyo ilipaswa kuwa na muundo wa N+V+Ts+T+N ambao ndiyo muundo sahihi kulingana na maneno aliyopewa.

Hata hivyo, watahiniwa 172,819 sawa na asilimia 12.79 walichagua kati ya vipotoshi B *Anapenda kula chakula mtoto wangu; C Mtoto wangu chakula anapenda kula; D Anapenda mtoto wangu kula chakula,* na *E Wangu mtoto anapenda chakula kula.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Anapenda kula chakula mtoto wangu* walishindwa kuelewa kuwa mpangilio huo wa maneno sio sahihi kwa sababu kiima hakiwezi kuchukua nafasi ya kiarifu katika sentensi. Pia, waliochagua kipotoshi *Mtoto wangu chakula anapenda kula* walishindwa kuelewa kuwa nomino “chakula” haiwezi kutokea baada ya kivumishi katika upande wa kiima

kwa kuzingatia muktadha wa sentensi husika, Vilevile, waliochagua kipotoshi *Anapenda mtoto wangu kula chakula* walishindwa kuelewa mpangilio huo wa kimuundo wa sentensi katika sarufi ya Kiswahili ambayo hujengwa na kiima na kiarifu. Aidha, waliochagua *Wangu mtoto anapenda chakula kula* walishindwa kuelewa kuwa kivumishi hakiwezi kufuatiwa na nomino katika kiima kwenye kuunda sentensi kwa sababu kivumishi huvumisha nomino; hivyo nomino ingetakiwa itangulie na kivumishi kifuate. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kutumia aina za maneno kwa usahihi kuunda sentensi kamili.

**Swali la 24:** Neno lipi **halilandani** na mengine kati ya yafuatayo?

A Mkuyu
B Msonobari
C Mkaratusi
D Waridi
E Mninga

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati kwenye lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 10 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 10: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 105,956 | 147,221 | 103,578 | 864,338 | 114,580 | 15,107 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 7.84 | 10.90 | 7.67 | 63.99 | 8.48 | 1.12 |


Jedwali Na. 10 linaonesha kuwa watahiniwa 864,338 sawa na asilimia 63.99 sawa na walichagua jibu sahihi D *waridi.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati kulingana na miktadha mbalimbali hivyo kuweza kubaini *waridi* ni mti wa maua unaonukia harufu nzuri na maneno mengine ni miti inayozalisha mbao.

Hata hivyo, watahiniwa 471,335 sawa na asilimia 34.89 walichagua kati ya vipotoshi A *Mkuyu*, B *Msonobari*, C *Mkaratusi* na E *Mninga.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *Mkuyu, Msonobari, Mkaratusi, na Mninga* walishindwa kuelewa maana na matumizi ya misamiati hiyo. Majina yote yana sifa inayofanana ambayo ni miti mikubwa na hutoa mbao. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walikosa umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 25:** Kulwa alikwenda nyumbani haraka _______ hakutaka kuchelewa. Neno lipi linafaa kukamilisha sentensi hii?

A kwa kuwa
B vilevile
C hata kama
D pamoja na
E kuliko

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 15 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 15:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 15 inaonesha kuwa watahiniwa 1,044,272 sawa na asilimia 77.31 walijibu vizuri swali hili kwa kuchagua A *kwa kuwa*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa juu ya viunganishi vyenye kuleta upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Watahiniwa hao waliweza kufahamu kuwa kiunganishi *kwa kuwa* huunganisha sentensi mbili zenye hadhi sawa kwa kuzingatia uhusiano wa maneno katika muktadha wa sentensi zote mbili.

Hata hivyo, watahiniwa 295,870 sawa na asilimia 21.90 walichagua kati ya vipotoshi B *vilevile*, C *hata kama*, D *pamoja na* E *kuliko.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *vilevile* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho hutumiwa kuunganisha dhana ya ziada. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *hata kama* walishindwa kuelewa kuwa hicho ni kiunganishi kinachounga dhana mbili zisizo na uhusiano. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *pamoja na* hawakuelewa kuwa hayo ni maneno yanayotumika kutaja vitu zaidi ya kimoja (nyongeza). Vilevile, uchaguzi wa kipotoshi *kuliko* ulitokana na watahiniwa hao kushindwa kuelewa kuwa kiunganishi hiki


hutumika kutofautisha au kulinganisha kitu kimoja na kingine. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya viunganishi ili kuleta upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

Katika swali la 26 hadi 30 maswali yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuonessha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*, katika umahiri mahususi wa kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

**Swali la 26:** Chombo maalum cha majini kinachotumika kuvusha watu na mizigo kwenda ng'ambo ya pili huitwaje?

A Winji
B Basi
C Pantoni
D Mkokoteni
E Garimoshi

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kama Chati Na. 16 inavyoonekana.




**Chati Na. 16:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*


Chati Na. 16 inaonesha kuwa watahiniwa 829,143 sawa na asilimia 61.38 walichagua jibu sahihi C *Pantoni.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu chombo cha majini kinachovusha watu na mzigo.

Hata hivyo, watahiniwa 507,060 sawa na asilimia 37.54 walichagua kati ya vipotoshi A *winji*, B *basi*, D *mkokoteni* na E *garimoshi*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *winji* hawakuelewa kuwa matumizi ya kifaa hiki ni kuvutia kamba ya nanga au kupakulia mizigo melini au jahazini. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *basi* hawakuelewa kuwa nano hilo lina maana ya gari kubwa la kuchukulia abiria. Waliochagua kipotoshi *mkokoteni* hawakuelewa kuwa neno hilo lina maana ya gari la kubebea mizigo linalosukumwa au kuburutwa. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *garimoshi* hawakuelewa kuwa neno hilo lina maana ya gari linalotembea juu ya reli lenye mabehewa mengi kwa ajili ya kubeba watu na mizigo. Kwa ujumla, watahiniwa hawa walikosa umahiri wa kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 27:** Mtu mwenye taaluma ya ujuzi wa kubuni, kutengeneza au kurekebisha majengo, barabara, madaraja au mitambo anaitwa nani?

A Rubani
B Dereva
C Mkutubi
D Mhandisi
E Mhunzi

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kama inavyoonekana katika Chati Na. 17.




**Chati Na. 17:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 17 inaonesha kuwa watahiniwa 581,667 sawa na asilimia 43.06 walichagua jibu sahihi D *mhandisi* kwa kuwa walikuwa na maarifa


ya kutosha ya kwamba *mhandisi* kuwa ni mtu mwenye ujuzi wa kubuni, kutengeneza au kurekebisha majengo, barabara, madaraja au mitambo.

Hata hivyo, watahiniwa 753,746 sawa na asilimia 55.08 walichagua kati ya vipotoshi A *rubani*, B *dereva*, C *mkutubi,* na E *mhunzi*. Uteuzi wa vipotoshi *rubani na dereva* ulitokana na kutokuelewa kuwa hao ni watu wenye ujuzi wa kuendesha vyombo vya usafiri. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *mkutubi* walishindwa kuelewa kuwa huyu ni mtu mwenye ujuzi wa kutunza vitabu katika maktaba. Uchaguzi wa kipotoshi *mhunzi* ulitokana na kutokuelewa kuwa neno hilo lina maana ya mtu mwenye ujuzi wa kufua vyuma. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 28:** Neno lipi kati ya yafuatayo lina maana sawa na neno "koroboi"?

A Taa
B Chemli
C Kibatari
D Karabai
E Mshumaa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa visawe vya maneno mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Muhtasari wa ufaulu umeoneshwa katika Chati Na. 18.




**Chati Na. 18:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 18 inaonesha kuwa watahiniwa 750,199 sawa na asilimia 55.54 walichagua jibu sahihi C *kibatari.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kwa kuelewa visawe vya maneno waliyopewa kwa kubaini maana ya neno hilo kuwa ni taa ndogo ya chupa au kopo yenye utambi inayotumia mafuta ya taa au dizeli.


Hata hivyo, watahiniwa 587,644 sawa na asilimia 43.05 walichagua kati ya vipotoshi A *taa,* B *chemli* D *karabai* na E *mshumaa*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *taa* hawakuelewa kuwa ni chombo kinachowashwa ili kimulike na kutoa mwanga. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *chemli* hawakuelewa kuwa ni kifaa chenye kutumia nishati ili kutoa mwanga. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *karabai* hawakuelewa kuwa ni taa yenye utambi wa kimia na inayotumia mafuta ya taa na kujazwa upepo. Aidha, waliochagua kipotoshi *mshumaa* hawakuelewa kuwa ni mche duara uliotengezwa kwa nta iliyogandishwa kwenye utambi wa pamba/kitambaa ili kumulikia usiku bila kutumia

nishati. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kuelewa visawe vya maneno mbalimbali.

**Swali la 29:** Mzee Kipeto alipokwenda kuwinda alifanikiwa kumuua "mbogo." Kisawe cha neno "mbogo" ni kipi kati ya vifuatavyo?

A Ndama
B Twiga
C Nyati
D Punda
E Pundamilia

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa visawe vya maneno mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kama Chati Na. 19 inavyoonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



**Chati Na. 19:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*


Chati Na. 19 inaonesha kuwa watahiniwa 1,044,225 sawa na asilimia 77.31 walichagua jibu sahihi C *nyati.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kisawe cha neno *mbogo* kuwa ni *Nyati* ambaye ni mnyama wa porini anayefanana na ng'ombe lakini mkubwa zaidi na mwenye pembe kubwa zilizopinda kuelekea mbele.

Hata hivyo, watahiniwa 294,876 sawa na asilimia 21.83 walichagua kati ya vipotoshi A *ndama*, B *twiga*, D *punda,* na E *pundamilia*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndama* hawakujua kuwa ni mtoto wa mnyama hasa ng'ombe na nyati. Waliochagua kipotoshi *punda* walishindwa kuelewa kuwa ni mnyama jamii ya farasi anayetumiwa zaidi kwa kukokota magari au kubeba mizigo. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *pundamilia* ulitokana na kutozingatia kuwa ni mnyama anayefanana na punda lakini mwenye miraba/mistari//milia myeusi na myeupe mwili mzima. Kadhalika, kipotoshi *twiga* walishindwa kuelewa kuwa huyu ni mnyama mrefu wa rangi ya kahawia na mwenye shingo ndefu. Hivyo, kutokana na maana ya vipotoshi hivyo; imebainika kuwa watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kuelewa visawe mbalimbali vya maneno.

**Swali la 30:** Neno lipi kati ya yafuatayo ni sahihi kutoka katika silabi "haborai" zilizochanganywa?

A Baharia
B Baharini
C Habarini
D Boharia
E Bohari

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuunda neno kutokana na silabi zilizochanganywa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 20 inavyoonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 20:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 20 inaonesha kuwa, watahiniwa 771,567 sawa na asilimia 57.12 walichagua jibu sahihi D *boharia.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu uundaji wa maneno mapya kwa kubadili mpangilio wa herufi na silabi. Watahiniwa hao walibaini kuwa mpangilio sahihi wa herufi zilizochanganywa unaunda neno hilo lenye maana ya mtu anayefanya kazi ya kutunza vifaa au bidhaa katika bohari.

Hata hivyo, watahiniwa 563,855 sawa na asilimia 41.74 walichagua kati ya vipotoshi A *baharia*, B *baharini*, C *habarini,* na E *bohari*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *baharia*, *baharini* na *habarini* hawakuwa na uelewa kuwa katika neno baharia herufi “o” imedondoshwa. Pia, katika

maneno *baharini* na *habarini* kumeongezwa silabi {ni} ambayo haipo katika neno lililochanganywa herufi “haborai”. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *bohari* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hiki kimedondosha herufi “a” kutoka katika silabi zilizochanganywa ambapo ni kinyume na taratibu za uundaji wa neno. Kwa jumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuunda maneno mapya kwa kubadili mpangilio wa herufi na silabi ili kukunda neno lenye maana.

Swali la 31 hadi 33 maswali yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*, katika umahiri mahususi wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.

**Swali la 31:** “Ungalifika mapema ______ ndugu yako.” Ni neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A Usingemkuta
B Ungemkuta
C Usingalimkuta
D Ungelimkuta
E Ungalimkuta

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 11 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 54,264 | 254,980 | 60,750 | 159,269 | 809,707 | 11,810 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya Watahiniwa | 4.02 | 18.88 | 4.50 | 11.79 | 59.94 | 0.87 |

Jedwali Na. 11 linaonesha kuwa, watahiniwa 809,707 sawa na asilimia 59.94 walichagua jibu sahihi E *ungalimkuta.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kuelewa matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Hivyo, waliweza kubaini muundo sahihi wa sentensi. Aidha, waliweza kuelewa kuwa kama sehemu moja ya sentensi shurutia ikiundwa na viambishi shurutishi **-ngali-** ni lazima upande wa pili wa sentensi hiyo ikamilishwe na viambishi shurutishi hivyo katika vitenzi.

Hata hivyo, watahiniwa 529,253 sawa na asilimia 39.18 walichagua kati ya vipotoshi A *usingemkuta*, B *ungemkuta*, C *usingalimkuta,* na D *ungelimkuta.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *usingemkuta* walishindwa kubaini kuwa neno hilo halina upatanisho wa kisarufi -nge- na lina kiambishi cha ukanushi *si-* katika neno walilopewa. Pia, waliochagua kipotoshi *ungemkuta* hawakubaini kuwa neno hilo lina upatanisho wa kisarufi -nge- ambalo halitumiki pamoja na -ngali- katika sentensi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *usingalimkuta* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina ukanushi -*si*- tofauti na matakwa ya swali. Aidha, waliochagua kipotoshi *ungelimkuta* hawakuelewa kuwa kipotoshi hiki hakina upatanisho wa kisarufi *-ngeli-* kwa kuzingatia sentensi iliyotolewa. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

**Swali la 32:** "Bibi aliangusha mzigo wa kuni ________ alijikwaa." Neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A Isipokuwa

B Ijapokuwa

C Kisha

D Lakini

E Kwa kuwa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 12 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 63,301 | 103,406 | 138,040 | 164,441 | 869,224 | 12,368 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 4.69 | 7.66 | 10.22 | 12.17 | 64.35 | 0.92 |

Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa, watahiniwa 869,224 sawa na asilimia 64.35 walichagua jibu sahihi E *kwa kuwa.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

Hata hivyo, watahiniwa 469,188 sawa na asilimia 34.73 walichagua kati ya vipotoshi A *isipokuwa*, B *ijapokuwa*, C *kisha,* na D *lakini*. Watahiniwa

waliochagua kipotoshi *isipokuwa* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo hutumiwa kuelezea jambo lililo mbali na jingine. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ijapokuwa* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo huashiria walakini katika jambo fulani.

Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kisha*, walishindwa kuelewa kuwa neno hilo huonesha jambo linalofuata baada ya kitu kingine. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *lakini* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo huonesha hitilafu au kasoro ya jambo au dosari. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya maneno katika dhima ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

**Swali la 33:** Chasaka aliamua kucharaza maneno wakati anamjibu baba yake. Nahau “charaza maneno” kama ilivyotumika katika sentensi hii ina maana ipi?

A Wasiliana kwa vitendo vya haraka

B Ongea haraka haraka kama cherehani

C Zungumza kwa kutafuna maneno

D Sema haraka haraka kwa nia ya kudanganya

E Ongea haraka haraka kwa nia ya kufurahisha

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa maana ya nahau katika miktadha mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kama jedwali Na. 13 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 135,367 | 371,781 | 176,765 | 561,398 | 89,784 | 15,685 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya Watahiniwa | 10.02 | 27.52 | 13.09 | 41.56 | 6.65 | 1.16 |

Jedwali Na. 13 linaonesha kuwa, watahiniwa 561,398 sawa na asilimia 41.56 walichagua jibu sahihi D *sema harakaharaka kwa nia ya kudanganya.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya nahau na maana zake katika sentensi.

Hata hivyo, watahiniwa 773,697 sawa na asilimia 57.28 walichagua kati ya vipotoshi A *Wasiliana kwa vitendo vya haraka*; B *Ongea haraka haraka kama cherehani*; C *Zungumza kwa kutafuna maneno* na E *Ongea haraka haraka kwa nia ya kufurahisha*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *wasiliana kwa vitendo vya haraka* na *ongea harakaharaka kama cherehani* walishindwa kuelewa kuwa vitendo na uzungumzaji wa haraka haviendani na usemaji wenye nia ya kudanganya. Vilevile, waliochagua kipotoshi *zungumza kwa kutafuna maneno* hawakuelewa kuwa hii ni nahau yenye maana ya kusema bila kutamka maneno vizuri kinyume na matakwa ya swali. Aidha, waliochagua kipotoshi *ongea harakaharaka kwa nia ya kufurahisha* hawakuelewa kuwa neno *kufurahisha* halina maana sawa na *kudanganya* kama swali lilivyohitaji. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nahau mbalimbali na maana zake katika sentensi.

Swali la 34 hadi 40, yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali,* hususani umahiri mahususi wa kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali.

**Swali la 34:** "Humu __________ wanamoishi panya wanaokula nguo." Neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A Ndipo

B Ndiko

C Ndimo

D Ndicho

E Ndio

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 14 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 14: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 159,969 | 59,674 | 999,059 | 40,625 | 79,380 | 12,073 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 11.84 | 4.42 | 73.96 | 3.01 | 5.88 | 0.89 |

Jedwali Na. 14 linaonesha kuwa, watahiniwa 999,059 sawa na asilimia 73.96 walichagua jibu sahihi C *ndimo.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika hali ya uyakinishi katika sentensi zenye kuonesha mahali watu walipo au vitu vilipo.

Hata hivyo, watahiniwa 339,648 sawa na asilimia 25.15 walichagua kati ya vipotoshi A *ndipo*, B *ndiko*, D *ndicho, na* E *ndio.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndipo* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho

kinaonesha mahali ambapo ni karibu. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndiko* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho kinadokeza mahali mbapo ni mbali. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndicho* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho kinadokeza urejeshi wa mtenda. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndio* hawakuelewa kuwa kipotoshi hicho ni kitenzi kishirikishi. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 35:** "Watu wengi wamejenga nyumba zao __________ ya barabara kuu." Neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A Katikati

B Kando

C Juu

D Chini

E Nyuma

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kama inavyoonekana katika jedwali Na. 15.

**Jedwali Na. 15: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 81,325 | 1,111,919 | 55,230 | 43,697 | 49,423 | 9,186 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 6.02 | 82.32 | 4.09 | 3.23 | 3.66 | 0.68 |

Jedwali Na. 15 linaonesha kuwa, watahiniwa 1,111,919 sawa na asilimia 82.32 walichagua jibu sahihi B *kando.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutumia upatanisho wa kisarufi kwa ufasaha. Aidha, waliweza kuelewa maana ya neno *kando* kuwa ni mahali palipo jirani na watu au vitu au mahali pengine hivyo kujibu kwa kufuata matakwa ya swali.

Hata hivyo, watahiniwa 229,675 sawa na asilimia 17.00 walichagua kati ya vipotoshi A *katikati,* C *juu*, D *chini* na E *nyuma.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *katikati*, *juu* na *chini* walishindwa kuelewa kuwa si rahisi nyumba kujengwa katika sehemu hizo za barabara kulingana na muktadha wa swali husika. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *nyuma* hawakuwa na uelewa kuwa barabara haina mbele wala nyuma. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia upatanisho wa kisarufi kulingana na miktadha mbalimbali.

## 1.2 SEHEMU B: Utungaji

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (36 - 40) yaliyohusu kifungu cha maneno na watahiniwa walitakiwa kutumia weledi na umahiri mkubwa waliokuwa nao kukamilisha kifungu cha maneno walichopewa kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku. Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

Kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku, jibu swali la 36-40 kwa **kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako ya kujibia ili kukamilisha kifungu cha maneno kifuatacho:

| | | | |
|---|---|---|---|
| A mizinga | B kiapo | C nchi jirani | D Makamu wa Rais |
| E waliwasili | | | |

*Ilipofika saa nne asubuhi viongozi (36) _________ ndani ya Uwanja wa Jamhuri. Kisha wakafuata viongozi wa (37) _________. Ilipofika saa nne na nusu asubuhi (38) _________ aliwasili na kupokelewa kwa shangwe na nderemo. Baadaye, mtangazaji alitutangazia kuwa Rais atawasili muda wowote kuanzia sasa. Punde si punde, Rais aliingia akiwa kwenye gari la wazi akiongozana na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Sote tulisimama na kuanza kushangilia huku vifijo vikisikika kutoka kila upande. Baada ya kuzunguka uwanja akiwasalimia wananchi, Rais alishuka kwenye gari na kuelekea sehemu maalum kwa ajili ya kupigiwa (39) ___________ ishirini na mmoja. Kisha akaenda kwenye meza maalum kwa ajili ya kula (40) ____________.*


Katika kujibu maswali haya, watahiniwa walitakiwa kukamilisha kifungu cha habari kama ifuatavyo**:**

| 36 | 37 | 38 | 39 | 40 |
|---|---|---|---|---|
| E | C | D | A | B |

Uchambuzi wa kina wa majibu ya watahiniwa katika kila swali (36 - 40) ni kama ifuatavyo:

**Swali la 36**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kukamilisha kifungu cha maneno alichopewa kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kama Chati Na. 21 kinavyoonesha.





**Chati Na. 21:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 21 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,130,118 sawa na asilimia 83.66 walichagua jibu sahihi E *waliwasili.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kukamilisha kifungu cha maneno. Hivyo, waliweza kubaini kuwa neno hilo hukamilisha sentensi ya kwanza katika kifungu cha maneno kwa kuzingatia muktadha pamoja na upatanisho wa kisarufi.

**Swali la 37**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika neno litakalokamilisha maelezo kuhusu viongozi waliofuata kuwasili uwanjani. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kama inavyoonekana katika Chati Na. 22.





**Chati Na. 22:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 22 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,047,540 sawa na asilimia 77.55 walichagua jibu sahihi, C *nchi jirani*. Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu hilo kutokana na muktadha wa swali husika ambao unazingatia mtiririko fasaha wa msuko wa matukio kwa kuangalia upatanisho wa kisarufi.

**Swali la 38**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini kiongozi mwingine aliyewasili ndani ya uwanja wa Jamhuri. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 23 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.





**Chati Na. 23:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 23 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,047,540 sawa na asilimia 77.55 walichagua jibu sahihi D *Makamu wa Rais.* Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu hilo kutokana na kuwapo kwa maneno yenye uhusiano wa jibu hilo kama vile *ilipofika saa nne na nusu asubuhi* ambapo kulihitaji nomino ili kukamilisha sentensi husika. Aidha, muktadha husika ulichangia mtahiniwa kujua jibu sahihi kwa kuwa kiitifaki, makamu wa Rais humtangulia Rais kufika katika hafla.

**Swali la 39**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini kitu alichofanyiwa Rais baada ya kuingia uwanjani na kwenda sehemu maalmu. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 24 inaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.





**Chati Na. 24:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 24 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,001,407 sawa na asilimia 74.14 walichagua A *mizinga.* Watahiniwa hao waliweza kubaini jibu hilo kutokana na kuwapo kwa kitenzi elekezi *kupigiwa* ambapo kulihitajika nomino ili kukamilisha sentensi kulingana na muktadha husika. Vilevile, kulikuwa na maneno mengine yaliyochangia mtahiniwa kuchagua jibu hilo kama vile, *ishirini na mmoja*. Maneno hayo yapo katika mstari wa swali husika.

**Swali la 40**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini tukio lililofuata ndani ya uwanja wa Jamhuri baada ya Rais kuwasili na kupigiwa mizinga. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kama inavyoonekana katika Chati Na. 25.




**Chati Na. 25:** *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Chati Na. 25 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,034,326 sawa na asilimia 76.57 walichagua jibu sahihi B *kiapo*. Watahiniwa hao waliweza kubaini jibu hilo kutokana na upatanisho wa kisarufi katika sentensi kwenye swali ambapo neno *kula* limekuwa ni kitenzi elekezi kwa jibu husika.

### 1.3 SEHEMU C: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (41 - 45) kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma* hususani umahiri mahususi wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. Mtahiniwa alitakiwa kutumia umahiri na weledi katika kusoma kwa makini na kuelewa shairi kisha kujibu maswali kutokana na shairi hilo. Lifuatalo ni shairi walilopewa watahiniwa.

*Acha mwanangu uache, uzembe uishilie,*
*Acha usiwe* ***kicheche****, mauti sisalimie,*
*Acha usiwe pekeche, upole ukimbilie,*
*Acha mwanangu uache, acha uishi salama*.


*Acha huo udokozi, takufa bure bileshi,*
*Acha pia uchochezi, utalamba matapishi,*
*Acha huo uchokozi, acha na huo ubishi,*
*Acha mwanangu uache, acha uishi salama.*

*Acha* ***benua kidari****, majuto ni mjukuu,*
*Acha usitakabari, usikie la mkuu,*
*Acha hayo machachari, utavunjika mguu,*
*Acha mwanangu uache, acha uishi salama.*

*Acha na huo mdomo, kazi kupiga umbea,*
*Acha na hiyo migomo, utaikosa bembea,*
*Acha usione shimo, ukakosa kutembea,*
*Acha mwanangu uache, acha uishi salama*


**Swali la 41:** Unaelewa nini mshairi anaposema “acha kubenua kidari?”

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya kauli *acha kubenua kidari* kama ilivyotumika katika shairi alilosoma. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Chati Na. 26 inaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 41.





**Chati Na. 26:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Chati Na 26 inaonesha kuwa watahiniwa 1,052,987 sawa na asilimia 77.97 walishindwa kujibu kwa usahihi swali husika. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini maana ya kauli kutokana na kutokuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma shairi na kubaini mawazo yaliyomo katika shairi husika. Baadhi yao waliandika majibu kama vile, *majuto ni mjukuu* kwa sababu ni maneno yaliyofuata katika kipande cha pili kwenye ubeti wa tatu wa shairi. Watahiniwa wengine waliandika *kugeuza kifua* kwa kuhusisha na nahau *kubenua kidari.* Wengine waliandika *ni sehemu ya kiungo cha kuku*. Watahiniwa walihusianisha neno *kidari* na kiungo cha kuku bila kuzingatia muktadha na lugha ya picha ya nahau husika. Wengine waliandika kuwa *ni kuvimbisha au kubinua kifua*. Kwa ujumla, watahiniwa waliandika majibu yao kwa kuzingatia umbo la nje la nahau husika badala ya maana inayobebwa na lugha ya picha katika nahau. Kielelezo Na. 1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


SWALI LA 41 kupiga umbea

**Kielelezo Na. 1** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 41*

Hata hivyo, watahiniwa 297,499 sawa na asilimia 22.02 waliweza kubaini maana ya nahau *acha kubenua kidari* kama ilivyotumika katika shairi. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kusoma shairi na kubaini maudhui yaliyomo. Hivyo, waliweza kutoa majibu sahihi kwa kuhusianisha maana ya nahau husika na muktadha pamoja na lugha ya picha iliyotumika katika shairi husika kama vile, *kuacha kujifanya unajua kila kitu, kuacha ukaidi, kuacha tabia ya kutosikiliza maelekezo ya wakubwa* au *kutokuwa msikivu*. Hii inathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa na mawanda mapana kuhusu nahau mbalimbali za lugha ya Kiswahili na maana zake. Kielelezo Na. 2 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa aliyepata alama zote.



SWALI LA 41
Ninaelewa kuwa niache tabia ya kujifanya najua sana kuliko wengine

**Kielelezo Na. 2:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 41*

**Swali la 42:** Katika ubeti wa pili, mshairi anabainisha athari ipi kwa watu wenye tabia ya wizi?


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha athari wanazozipata watu wenye tabia ya wizi kama ilivyobainishwa katika ubeti wa pili wa shairi alilosoma. Kiwango cha ufaulu katika swali hili

kilikuwa kizuri. Chati Na. 27 inaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali.




**Chati Na. 27:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*


Chati Na 27 inaonesha kuwa watahiniwa 888,119 sawa na asilimia 65.77 waliweza kubainisha athari inayowapata watu wenye tabia ya wizi kuwa ni *kifo (kufa,kupoteza maisha,uhai).* Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma shairi. Hivyo, walielewa beti za ushairi pamoja na maudhui yake. Kielelezo Na. 3 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa aliyepata alama zote.




**Kielelezo Na. 3:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 42*

Hata hivyo, watahiniwa 462,367 sawa na asilimia 34.24 walishindwa kubaini athari inayowapata watu wenye tabia ya wizi kotoka katika ubeti wa pili. Watahiniwa hao hawakuelewa maudhui yaliyomo katika shairi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika majibu kama vile; *benua*


*kidali, majuto ni mjukuu, uishi salama*, *utavunjika mguu, udokozi, uchochezi* na *uchokozi*. Kielelezo Na. 4 kinaonesha jibu ambalo sio sahihi.




**Kielelezo Na. 4:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 42*

**Swali la 43:** Nini maana ya neno "kicheche" kama lilivyotumika katika ubeti wa kwanza?


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya neno *kicheche* kama lilivyotumika katika ubeti wa kwanza. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Chati Na. 28 inaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali.




**Chati Na. 28**`: *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Chati Na. 28 inaonesha kuwa watahiniwa 940,425 sawa na asilimia 69.64 walishindwa kujibu swali kwa usahihi. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya msamiati huo kwa kukosa maarifa


kuhusu maana ya neno hilo na jinsi lilivyotumika katika muktadha wa shairi husika. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitoa majibu kama vile: Mtu mwenye tabia ya kupenda wanawake, kipande kidogo cha moto, kuwa na pesa nyingi, mtu anayejipenda na kujithamini pamoja na kuwa mlevi wa pombe. Kielelezo Na. 5 kinaonesha jibu la mtahiniwa lisilo sahihi.


SWALI LA 43

Mtu anayetumwa Kupeleka Ujumbe au taarifa.

**Kielelezo Na. 5:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 43*

Hata hivyo, watahiniwa 410,061 sawa na asilimia 30.36 waliweza kutoa maana ya neno “kicheche” kuwa ni *mtu mwenye tabia mbaya kama vile, udokozi, uchokozi, uchochezi, au umbea*. Watahiniwa hao walitoa jibu hilo kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati *kicheche* kama ulivyotumika katika ubeti wa kwanza wa shairi kwa kuzingatia muktadha na lugha ya picha iliyotumika. Kielelezo Na. 6 kinaonesha jibu sahihi la mtahiniwa katika swali husika.


SWALI LA 43


kicheche ni mtu mwenye tabia ya wizi

**Kielelezo Na. 6:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 43*

**Swali la 44**: Mshairi anaposema “acha na huo mdomo” anawaonya watu wenye tabia gani katika jamii?


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini tabia za watu wanaoonywa na mshairi kutokana na kauli *acha na huo mdomo*.

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuli sana. Chati Na. 29 inaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali.




**Chati Na. 29***: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*


Chati Na. 29 inaonesha kuwa watahiniwa 1,113,262 sawa na asilimia 82.44 waliweza kujibu kwa usahihi swali. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma kwa makini na kuelewa maudhui yaliyomo katika shairi. Watahiniwa hao waliweza kuelezea tabia za watu wanaoonywa na mshairi kutokana na kauli “acha na huo mdomo” kuwa ni *watu wenye tabia ya kuwasema watu wengine, kuwasengenya pamoja na umbea.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya misemo ya lugha ya kishairi na jinsi ilivyojengwa kwa lugha ya picha. Kielelezo Na. 7 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44.


SWALI LA 44

MSHAIRI ANAWAONYA WATU WALIO WAMBEA KATIKA JAMII ASEMAPO "ACHA NA HUO MDOMO"

**Kielelezo Na. 7:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44*


Hata hivyo, watahiniwa 237,224 sawa na asilimia 17.57 walishindwa kuandika tabia za watu wanaoonywa na mshairi kutokana na kauli husika. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa maudhui yaliyomo katika kauli husika kwenye shairi. Mfano, baadhi ya watahinwa waliandika *punguza kiburi, ujeuri, udokozi, tabia ya wizi* na *acha uishi salama*. Watahiniwa hao walitoa majibu bila kufuata matakwa ya swali kwa kuwa maneno hayo hayadokezi tabia za watu wanaoonywa na mshairi kutokana na kauli husika. Kielelezo Na. 8 kinaonesha jibu lililo sahihi la mtahiniwa katika swali husika.




**Kielelezo Na. 8:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 44*


**Swali la 45:** Mwandishi wa shairi hili anatoa ujumbe gani katika jamii?

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,350,780 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini ujumbe uliotolewa na mshairi kwa jamii. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 30 inaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali.




**Chati Na. 30:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*


Chati Na. 30 inaonesha kuwa watahiniwa 961,571 sawa na asilimia 71.20 waliweza kujibu kwa usahihi swali. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa ujumbe uliomo kwenye shairi. Aidha, waliweza kutoa ujumbe uliofikishwa na mshairi kwa jamii kuwa ni *kuacha tabia mbaya ya wizi, umbea, kiburi, udokozi, uzembe, uchochezi na migomo.* Pia*,* mshairi alisisitiza ujumbe wa kuwa na *tabia ya kiungwana*. Kielelezo Na. 9 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.




**Kielelezo Na. 9***: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 45*

Hata hivyo, watahiniwa 388,915 sawa na asilimia 28.80 walishindwa kuandika ujumbe uliotolewa na mshairi. Baadhi yao waliandika majibu

kama vile, *acha mwanangu uache, acha uishi salama* kwa sababu mstari huu umerudiwa katika kila ubeti. Pia, watahiniwa wengine waliandika *kubinua kidari*, *kuwa kicheche* na *kulamba matapishi*. Uandishi wa majibu hayo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa ujumbe uliomo katika shairi walilosoma. Kielelezo Na. 10 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi.


SWALI LA 45 benua kibatari

**Kielelezo Na. 10:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 45*

## 2.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI

Umahiri uliotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali*, kutumia *msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali, kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali, kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza, kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma,* na *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali*.

Uchambuzi unaonesha kuwa umahiri uliokuwa na kiwango cha juu zaidi ni *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza (82.49%),* ikifuatiwa na *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali* (77.97%), *kutumia msamiati katika kuzungumza*

*kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali* (63.63%), na *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali*

(61.72%). Umahiri wa *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali* na *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma* zilikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 58.88 na 54.70 mtawalia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, maswali matano kati ya maswali saba katika umahiri wa *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza* yalijibiwa vizuri zaidi. Maswali hayo ni swali la 3 (90.39%), 5 (86.47), 1 (85.68%), 2 (82.17%) na 4 (80.81). Katika umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali*, swali la 8 lilijibiwa vizuri zaidi na kuwa na ufaulu wa asilimia 82.15. Aidha, swali la 11, 15 na 18 yalijibiwa vizuri ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa zaidi ya asilimia 71.99, 71.59 na 78.45 mtawalia. Pia, katika umahiri wa *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali,* maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ni swali la 35 (82.32%) na 36 (83.66%). Katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali,* swali la 23 ndilo lililojibiwa vizuri zaidi na kuwa na asilimia 86.50. Vilevile, katika umahiri wa *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma,* swali la 44 lilikuwa na ufaulu wa juu zaidi wa asilimia 82.42. Aidha, katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali,* swali la 30 lilikuwa na ufaulu wa juu wa asilimia 77.31 kuliko maswali mengine katika umahiri husika.

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mahiri zilizotahiniwa kwa mwaka 2021 na 2022 kinaonesha kushuka kwa baadhi ya umahiri na

kupanda kwa aina zingine za umahiri zilizotahiniwa mwaka 2022. Viwango vya ufaulu katika mwaka 2022 vikilinganishwa na mwaka 2021 vinaonesha kuwa, katika umahiri wa *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma,* kiwango cha ufaulu kimepungua kutoka asilimia 69.90 hadi asilimia 54.70; hivyo ufaulu umeshuka kwa asilimia 15.20. Pia, katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali*, kiwango cha ufaulu kimepungua kutoka asilimia 61.30 hadi 58.88 hivyo kushuka kwa asilimia 2.42. Vilevile, katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali* ufaulu umeshuka kwa asilimia 4.57 kutoka asilimia 68.20 hadi 63.63. Aidha, ufaulu umepanda katika umahiri wa *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza* kwa asilimia 6.39 kutoka asilimia 76.10 hadi 82.49. Pia, katika umahiri wa *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali*, kiwango cha ufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 63.70 hadi 77.97 sawa na asilimia 14.27. Vilevile, katika umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali* ufaulu umepanda kwa asilimia 3.92 kutoka asilimia 57.80 hadi 61.72. Kiwango cha ufaulu katika kila umahiri kimeoneshwa katika kiambatisho cha pekee.

## 3.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa umahiri unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili mwaka 2022 kilikuwa kizuri (66.56%). Vilevile, uchambuzi huu umebainisha changamoto zilizowafanya watahiniwa kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Miongoni mwa changamoto hizo ni; kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu msamiati, kauli taarifa na kauli halisi, upatanisho wa kisarufi, aina za maneno pamoja na kushindwa kujibu

maswali ya ushairi kikamilifu. Dosari nyingine ni kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo, au kutojibu kabisa maswali pamoja na kutofuata taratibu za kusiliba fomu za OMR inavyotakiwa.

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha ufaulu zaidi wa wanafunzi katika aina za umahiri uliokuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani yafuatayo yanapendekezwa:

(i) Katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali, walimu watumie mbinu ya bungua bongo, kazi mradi na maigizo kufundisha kauli taarifa na kauli halisi na kuwaelekeza wanafunzi mambo muhimu ya kuzingatia (sifa) wakati wa utokeaji wa kauli hizo. Hii itawajengea wanafunzi umahiri wa kutambua kauli hizo.

(ii) Katika umahiri wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma, walimu wafundishe wanafunzi misingi madhubuti ya kusoma kimya na kwa sauti kifungu cha habari na kujibu maswali kwa usahihi. Walimu watumie mbinu ya kuwaweka wanafunzi katika vikundi mbalimbali na kusomeana matini kwa sauti katika vikundi vyao. Ufundishaji huo utawawezesha wanafunzi kuwa mahiri katika kuelewa maudhui ya habari.

(iii) Katika umahiri wa kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali, walimu wanatakiwa kufundisha wanafunzi kwa kutumia njia shirikishi (vikundi) na igizo dhima kubainisha sifa za aina za maneno na dhima zake katika sentensi ili kuwajengea wanafunzi umahiri wa kutumia aina mbalimbali za maneno katika sentensi.

(iv) Katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali, walimu wanatakiwa kutumia njia ya vikundi na bungua bongo kufundishia visawe vinavyotumika katika mazingira yao kwa kusoma na kusikiliza matini mbalimbali.

(v) Katika umahiri wa kusoma shairi na kubaini maudhui yaliyomo, walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa mashairi kwa kuzingatia muundo wake ikiwa ni pamoja na maana ya

msamiati, nahau na lugha za picha kwa kuzingatia muktadha wa shairi husika. Ili kufanikisha hayo mwalimu anaweza kutumia mbinu shirikishi (majadiliano) na kazi mradi hasa kwa wanafunzi kutunga mashairi ya kisasa na kimapokeo kadri wawezavyo.

(vi) Katika umahiri wa kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza, wanafunzi wanatakiwa kufanya mazoezi ya kusikiliza mazungumzo au hadithi kutoka kwa wazungumzaji au wasimuliaji wenye lafudhi tofauti. Vilevile, wapewe mazoezi ya kusikiliza taarifa mbalimbali za habari. Kadhalika, wanafunzi wapewe mazoezi ya kusikiliza habari fulani katika mazingira yenye kelele ili wazoee kumakinika na kile wanachopaswa kusikiliza.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

**ULINGANIFU WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA UMAHIRI KATIKA PSLE 2021 NA PSLE 2022**

| Na. | Umahiri | Mtihani wa 2021 | | | | Mtihani wa 2022 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. | 1 | 91.6 | 76.1 | Vizuri | 1 | 85.68 | 82.49 | vizuri |
| | | 2 | 90.0 | | | 2 | 82.17 | | |
| | | 3 | 53.8 | | | 3 | 90.39 | | |
| | | 4 | 90.7 | | | 4 | 80.81 | | |
| | | 5 | 67.6 | | | 5 | 86.47 | | |
| | | 6 | 68.8 | | | 6 | 73.74 | | |
| | | 7 | 70.3 | | | 7 | 78.17 | | |
| 2. | Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. | 20 | 81.2 | 69.9 | Vizuri | 31 | 59.94 | 54.70 | Wastani |
| | | 21 | 50.5 | | | 32 | 64.35 | | |
| | | 22 | 88.4 | | | 33 | 41.56 | | |
| | | 41 | 57.8 | | | 41 | 22.03 | | |
| | | 42 | 85.8 | | | 42 | 65.76 | | |
| | | 43 | 44.5 | | | 43 | 30.36 | | |
| | | 44 | 88.9 | | | 44 | 82.42 | | |
| | | 45 | 62.3 | | | 45 | 71.19 | | |
| 3. | Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali. | 23 | 66.7 | 68.2 | Vizuri | 20 | 40.79 | 63.63 | Vizuri |
| | | 24 | 57.7 | | | 21 | 53.67 | | |
| | | 25 | 78.9 | | | 22 | 59.53 | | |
| | | 26 | 88.7 | | | 23 | 86.50 | | |
| | | 27 | 73.2 | | | 24 | 63.99 | | |
| | | 28 | 44.1 | | | 25 | 77.31 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. | 34 | 72.7 | 63..7 | Vizuri | 34 | 73.96 | 77.97 | vizuri |
| | | 35 | 25.9 | | | 35 | 82.32 | | |
| | | 36 | 65.1 | | | 36 | 83.66 | | |
| | | 37 | 52.9 | | | 37 | 77.55 | | |
| | | 38 | 86.0 | | | 38 | 77.60 | | |
| | | 39 | 56.1 | | | 39 | 74.14 | | |
| | | 40 | 87.5 | | | 40 | 76.57 | | |
| 5. | Kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. | 29 | 59.5 | 61.3 | Vizuri | 26 | 61.38 | 58.88 | Wastani |
| | | 30 | 71.7 | | | 27 | 43.06 | | |
| | | 31 | 39.8 | | | 28 | 55.54 | | |
| | | 32 | 86.9 | | | 29 | 77.31 | | |
| | | 33 | 48.6 | | | 30 | 57.31 | | |
| 6 | Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | 8 | 39.4 | 57.8 | Wastani | 8 | 82.15 | 61.72 | Vizuri |
| | | 9 | 47.8 | | | 9 | 56.10 | | |
| | | 10 | 70.5 | | | 10 | 65.09 | | |
| | | 11 | 51.3 | | | 11 | 71.99 | | |
| | | 12 | 47.7 | | | 12 | 61.00 | | |
| | | 13 | 74.3 | | | 13 | 57.38 | | |
| | | 14 | 53.0 | | | 14 | 49.62 | | |
| | | 15 | 43.0 | | | 15 | 71.59 | | |
| | | 16 | 86.8 | | | 16 | 62.22 | | |
| | | 17 | 35.5 | | | 17 | 55.52 | | |
| | | 18 | 85.5 | | | 18 | 78.45 | | |
| | | 19 | 60.6 | | | 19 | 29.62 | | |